



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA NYANG'HWALE



Unapojibu tafadhali taja:

KUMB. NA. AC/18/214/51

Tarehe : 08/12/2022

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale anawatangazia Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi za kazi zifuatazo:-

### 1. WAZOA TAKA NAFASI NNE (04)

#### SIFA ZA MWOMBAJI

- i. Awe ni Mwananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale (Mkazi)
- ii. Awe na Kitambulisho cha NIDA
- iii. Awe na afya njema, mwaminifu, mwenye kujituma
- iv. Awe amepata Mafunzo ya mgambo
- v. Mwombaji awe ni Mtanzania asiezidi umri wa miaka 45
- vi. Mwombaji awe hajawahi kupatikana na kosa lolote la jinai, kufungwa jela au kupatikana na kosa lolote katika Utumishi wa Umma.
- vii. Barua zote za maombi zipitie kwa Mshauri wa Mgambo Wilaya ya Nyang'hwale

#### MAJUKUMU YA KAZI

- i. Usafirishaji/uondoaji taka ngumu
- ii. Kuzoa taka katika maeneo ya Wilaya ya Nyang'hwale
- iii. Kupeleka taka eneo la dampo
- iv. Kuhakikisha Trekta linakuwa safi na matunzo kwa ajili ya kazi

## 2. DEREVA WA MTAMBO (TREKTA) NAFASI (01)

### SIFA ZA MWOMBAJI

- i. Awe na Leseni daraja E au C1 ya uendeshaji wa Magari/Mtambo/Trekta ambayo amefanya kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali
- ii. Awe amehudhuria mafunzo ya uendeshaji Magari (Basic driving course yanayotolewa na Chuo cha mafunzo ya ufundi stadi (VETA) au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.
- iii. Waombaji wenye cheti cha majaribio ya ufundi Daraja II watafikiriwa kwanza..
- iv. Awe na uzoefu wa kutosha wa kuendesha Trekta
- v. Awe na kitambulisho cha NIDA.

### MAJUKUMU YA KAZI

- i. Usafirishaji/uondoaji taka ngumu kwenye maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Nyang'hwale
- ii. Kupeleka taka eneo la dampo
- iii. Kuhakikisha Trekta linakuwa safi na matunzo kwa ajili ya kazi
- iv. Kufanya kazi nyingine atakazo pangwiwa na Mwajiri


Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **13/12/2022 saa 9:30 alasiri**. Aidha maombi yote yawasilishwe kwa anuani ifuatayo;-

Mkurugenzi Mtendaji (W)

S. L.P 352

**NYANG'HWALE.**

Tangazo hili pia linapatikana katika Tovuti ya Halmashauri [www.nyang'hwaledc.go.tz](http://www.nyang'hwaledc.go.tz) na katika mbao za matangazo.

  
Husna T. Chambo  
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**  
**NYANG'HWALE**

**MKURUGENZI MTENDAJI**  
S.L.P 352.  
**NYANG'HWALE.**

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Nyang'hwale, S. L. P. 352, Mkoa wa Gelta, Barua pepe:ded@nyanghwaledc.go.tz  
Tovuti: [www.nyanghwale.go.tz](http://www.nyanghwale.go.tz)